

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI AWAMU YA PILI

Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania (TCU) inautangazia umma kuwa imekamilisha awamu ya kwanza ya uhakiki wa sifa za waombaji waliodahiliwa na taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2018/19. Majina ya waombaji waliochaguliwa katika awamu ya kwanza yameshatangazwa na vyuo husika.

Hata hivyo kutokana na waombaji wengi kutochaguliwa kutokana na sababu mbali mbali, Tume inatangaza kuwa imefungua dirisha la maombi awamu ya pili kuanzia tarehe 10 hadi 14 Septemba 2018 ili kuruhusu makundi yafuatayo kuomba udahili:

- Waombaji waliokosa nafasi kwenye awamu ya kwanza;
- Waombaji wa kidato cha sita na stashahada walioshindwa kuomba katika awamu ya kwanza;
- Waombaji waliomaliza mitihani ya “Cambridge” mwaka 2018 na matokeo yao yameshatoka; na
- Waombaji waliokuwa wamedahiliwa miaka ya nyuma na kuacha au kukatisha masomo.

Aidha Tume inapenda kuisitiza kuwa utaratibu wa kutuma maombi ni ule ule wa kutuma maombi moja kwa moja vyuoni kama ilivyokuwa katika awamu ya kwanza ya Udahili. *Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili yari potuwe moja kwa moja kwenye vyuo husika na siyo TCU.*

Imetolewa
na
Katibu Mtendaji
Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania
10/09/2018